Jina …… **Nambari Yako ……**

Sahihi …….

Tarehe ……

102/2
KISWAHILI
KARATASI YA 2
(LUGHA)
JULAI / AGOSTI 2009
MUDA: SAA $2^{1}/_{2}$

MITIHANI YA MAKADIRIO YA WILAYA YA BORABU - 2009

Kenya Certificate of Secondary Education (K.C.S.E)

102/2
KISWAHILI
KARATASI YA 2
(LUGHA)
MUDA: SAA 2 ½

MAAGIZO:

- Jibu maswali yote. Majibu yako yaandikwe katika nafasi zilizoachwa katika kijitabu hiki cha maswali

KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE

SWALI	**UPEO**	**ALAMA**
1	15	
2	15	
3	40	
4	10	
JUMLA	80	

Karatasi hii ina kurasa 8 zilizopigwa chapa, watahiniwa lazima wahakikishe kurasa zote zimepigwa chapa sawa sawa na kuwa maswali yote yamo.

1. **UFAHAMU**

Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali.

Licha ya kuwa na historia ya kiasi, maisha ya binadamu ni kioja kikubwa. Hebu jiulize jinsi uhai wako wewe mwenyewe ulivyoanza sembuse unavyoweza kupumua na kuishi siku nenda siku rudi.

Dini zimefahamisha kuwa sisi binadamu tumeumbwa na Mwenyezi Muumba. Hata hivyo Muumba hutumia mume na mke kutuanzishia maisha yetu humu duniani. Uhai wa hapa duniani huanzia katika tumbo la mwanamke muda mfupi tu baada ya mume na mke kushirikiana katika tendo la kujamiiana. Katika ngono hii yenye ufanisi, mbegu moja ya manii kutoka kwa mwanaume, hudunga na kujiingiza katika yai la mwanamke huku ikilirutubisha. Tangu hapo mtu huwa na mama akawa mjamzito. Hatua ya kwanza ya uhai!

Wanasayansi wametuthibitishia kuwa mbegu katika shahawa kutoka kwa mwanamume ina Kromosomu ishirini na tatu (23) nalo yai la mwanamke lina idadi iyo hiyo ya kromosomu. Basi katika hatua ya kwanza ya uhai wake, binadamu ana kromosomu arubaini na sita (46). Kromosomu hizo zote ndizo humfanya mtu kuwa mkamilifu kwa kukadiria mambo mbalimbali adhimu. Kwa mfano hukadiria kama kiumbe kitakuwa cha kike au cha kiume, mtu mweupe au mtu mweusi, mwerevu au wa akili chache, mwenye nywele za singa au za kipilipili, atakuwa na damu ya namna gani, michoro ya vidole vyake itakuwa vipi na hata utu wake utakuwa wa namna gani katika siku za usoni.

Elimu yote anayopata mtu kutoka kwa jamii na mazingira huweza tu kujenga juu ya yaliyo kwisha kuanzilishwa na Kromosomu katika yai lililorutubishwa tumboni

Haihalisi kabisa kufikiria kwamba katika hatua za mwanzo tumboni mwa mama kiumbe huwa katika hali ya ukupe. La hasha! Yeye hujitegemea kwa vyovyote na ana upekee wake. Hatangamani na mama yake. Roho yake humdunda mwenyewe na damu yake ambayo huenda ikawa tofauti kabisa na ya mama yake, humtembea na kumpiga mishipani mwake. Isitoshe, yeye si mojawapo katika viungo vya mwili wa mama yake vinavyomdhibiti katika himaya yake ndogo.

Amini usiamini, hapana binadamu hata mmoja ambaye amewahi kuwa sawa kimaumbile na mwingine na wala hatakuweko. Hata watoto pacha kutoka yai moja la mama hawawi sawa Lazima watatufautiana.Si nadra kusikia mtu amepata ajali akahitaji msaada wa damu na pakosekane kabisa mtu hata mmoja kutoka jamaa yake wa kumwauni. Basi ukistaajabu ya Musa utaona ya Firauni.

Maswali

a) Pendekeza kichwa kifaacho kwa taarifa uliyoisoma. (alama1)

……..

……..

b) 'Ngono yenye ufanisi" ina maana gani kwa mujibu wa taarifa? (alama2)

……..

……..

c) Uchunguzi wa sayansi umekita mizizi imani gani ya kidini? (alama2)

……..

……..

d) Taja majukumu yoyote matano yanayotekelezwa na kromosomu (alama5)

i) …….

ii) …….

iii) …….

iv) …….

v) …….

e) Toa sababu ya elimu ya kutoka kwa jamii na mazingira kuelekea kuwa bure ghali (alama2)

……

……..

……..

f) Eleza maana ya mafungu haya. (alama3)

i) Huwa katika hali ya ukupe ……..

ii) Himaya ……

iii) Hatangamani na mama yake ……

2. **UFUPISHO**

Soma makala kasha ujibu maswali.

Ugonjwa wa ukimwi umekuwa na bado ungali tishio kubwa kwetu. Mataifa mengi ya kiafrika yameathiriwa kwa sababu ya ugonjwa huu ambao umeangamiza kiasi kikubwa cha watu wenye nguvu katika jamii ambao ndio tegemeo la uzalishaji mali wa taifa. Matokeo yake ni watoto mayatima na vikongwe ambao wanajisabilia kuyakimu maisha ya wajukuu walioachwa na wazazi wao. Ingawa vita dhidi ya ugonjwa vimeleta ufanisi mkubwa, bado kuna masuala yanayohitaji kunyooshwa ili ushindi dhidi ya janga hili uweze kuwa kamilifu.

Licha ya mashirika mbalimbali kutambua na kujitolea kutoa mafunzo kuhusu umuhimu wa kuwakubali walioathiriwa na ugonjwa huu, bado kuna ubaguzi wanaofanyiwa wanaougua. Watu huwabagua kazini wanaougua ugonjwa huu. Hali hii huliua tumaini la watu hawa kuishi. Huwa wamenyimwa nafasi ya kupunguza makali ya ugonjwa huu, wenye watoto huwa hawana namna ya kuwakimu watoto wao na hata pesa za kununulia vyakula vinavyofaa huwa ni ndoto zilizopitwa na wakati. Vyombo vya habari hivi mjuzi vimeangazia kuhusu wazazi waliotishia

kuwaondoa watoto wao kutoka shule waliyokuwa wakisomea iwapo usimamizi wa shule hiyo ungedinda kuwafukuza watoto watatu waliougua ugonjwa wa ukimwi. Matokeo yake ni watoto hawa wadogo kutimuliwa shuleni humo. Huu ni ubaguzi ambao haufai kwa ndugu zetu.

MASWALI

a) Kwa kuzingatia mambo muhimu, fupisha aya ya kwanza (maneno 35 – 40),

(alama 6, 1 ya utiririko)

Maandalizi

……..
……..
……..
……..
……
……..
……..

Jibu

……..
……..
……..
……..
……
……..
……..

b) Fupisha aya ya mwisho kwa maneno 50 (alama 9, 2 utiririko)

Maandalizi

……..
……..
……..
……..
……
……..
……..

Jibu

……..

……..

……..

……..

……

……..

……..

……..

……

……..

……..

……..

3. MATUMIZI YA LUGHA

a) Ainisha silabi katika neno ‘mtumbwini’ (alama 2)

……..

……..

……..

……..

b) Tunga sentensi ukitumia neno ‘kijana’ kama :- (alama2)

i) Nomino

……..

……..

……..

……..

ii) Kivumishi

……..

……..

……..

……..

c) Changanua mofimu katika tungo:

Tutalima (alama2)

……..

……..

……..

……..

d) Tofautisha kati ya matumizi ya: (alama2)

i) enye …….

ii) enyewe …….

e) Tumia kiunganishi ‘wala’ katika sentensi ili kuonyesha matumizi yake (alama1)

……..

……..

……..

……..

f) Geuza kwa umoja

Mishale yao ilifungwa kwa manyoya meusi (alama2)

……..

……..

……..

……..

g) Kwa kutumia kiambishi ‘kwa’ tunga sentensi mbili kuonyesha matumizi ya

i) kusudi (alama2)

…….

ii) akisami

…….

h) Andika kwa wakati ujao hali timilifu.

Ugomvi ulikwisha na mama akarudi (alama2)

……..

……..

……..

……..

……..

……..

i) Nyambua vitenzi hivi kwa kauli ya kutendeshea (alama2)

i) pwa …….

ii) nya ……..

j) Tambua na ueleze aina ya virai: Mama mzee alikuwa akitembea (alama2)

……..

……..

……..

……..

k) Changanua sentensi hii kwa kielelezo cha mishale (alama4)
kitabu kizuri sana kimesomwa leo

……..
……..
……..
……..

l) Mamake alikuwa mkali. Yeye alikuwa mwanajeshi. Unganisha (alama2)

……..
……..
……..
……..

m) Toa maana mbili za sentensi hii:
Okiomeri alimpikia Gesare chakula (alama2)

……..
……..
……..
……..

n) "Sitaki na sitataka mtoto mkaidi kama wewe." Mzazi alisema.
Andika kwa usemi wa taarifa (alama2)

……..
……..
……..
……..

o) Yule nyoka alikatwa mkia. Geuza katika udogo (alama2)

……..
……..
……..
……..

p) Sikukula kabla ya kumkamua ng'ombe. Sahihisha. (alama2)

……..
……..
……..
……..

q) Kuku aliyeripotiwa kuibwa alipatikana katika chumba cha kulala.

Anza: Katika chumba cha kulala……. (alama2)

……..

……..

……..

……..

r) Mtoto mweusi ametabasamu sana.

Geuza kwa kinyume (alama2)

……..

……..

……..

……..

s) Ngeli ya mahali ina viambishi vitatu. Vitaje na ueleze matumizi yao (alama3)

4. **ISIMU – JAMII**

Huku ukitoa mifano halisia, fafanua sifa zozote tano za lugha inayotumiwa mkahawani.

(alama10)

……..

……..

……..

……..

……..

……..

……..

……..

……..

……..

……..

……..

……..

……..

……..

……..

……..

……..

……..

……..

……..

……..

……..